Kutembea Karibu Na Mungu
(A Closer Walk With God)

na

Ellis P. Forsman

Kutembea Karibu Na Mungu
(A Closer Walk With God)

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 8, 2011

Kutembea Karibu Na Mungu

Waeb. 5:12-14

Tunajua au kutofautisha kile ambacho ni kizuri au kibaya. Kujua utofauti haiji maramoja kwenye wokovu. Ni uwezo unaokuja na muda "na mazoezi"

Waeb. 5:12-14, *"Kwa maana iwapasapo kuwa waalimu (maana wakati mwingi umepita), mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu, nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu. Kwa maana kila mtu atumiaye maziwa hajui sana neno la haki, kwa kuwa ni mtoto mchanga. Lakini chakula kigumu ni cha watu watu wazima, ambao akili zao kwa kutumiwa, zimezoezwa kupambanua mema na mabaya."*

Somo hili limeundwa ilikutasaidia kuwa na uwezo kutofautisha, ili kwamba kweli tuwe "kutembea karibu na Mungu". Kuamua kilicho kizuri na kilicho kibaya hakika ni rahisi. Inajumlisha kuuliza maswali machache kuhusu swala lililopo.

Je kiuwazi Imepigwa Marufuku Katika Biblia?

Vituvingi vimeonyeshwa wazi kuwa ni makosa.

Orodha moja ya vitu hivyo inapatikana katika:

Wagal. 5:19-21, *"Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, fitina, hasira, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo, katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyo kwisha kuwambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawata urithi ufalme wa Mungu."*

Orodha kama hiyo inapatikana katika:

Waef. 5:3-7, *"Lakini uasherati usitajwe kwenu kamwe, wala uchafu wo wote wa kutamani, kama iwastahilivyo watakatifu; wala aibu wala maneno upuzi wala ubishi; hayo haya pendezi; bali afadhali kushukuru. Maana neno hili mnalijua hakika, ya kwamba hakuna mwasherati wala mchafu wala mwenye tamaa, ndiye mwabudu sanamu aliye na urithi katika ufalme wa Kristo na Mungu. Mtu asiwadanganye kwa maneno yasiyo na maana; kwa kuwa kwa sababu ya hayo hasira ya Mungu huwajia wana wa uasi. Basi msishirikiane nao."*

Kwa vitu vilivyoonyeshwa, inayo tuliza swala hili. Kidogo kutokana na wakristo wanavyo husika. Hakuna nafasi ya mjadala wakati maandiko yamezuia vitu kama hivyo.

Lakini siyo dhambi zote zimeonyeshwa kwa majina, Biblia ingekuwa haina mwisho kama hiyo ingekuwa ni kweli! Kwa hiyo swali lingine linapaswa kuulizwa.

Je Vinafanana Vitu Vilivyopigwa Marufuku Katika Biblia?

Katika Wagal. 5:19-21, angalia neno *"mambo ya jinsi hiyo".*

Wagal. 5:19-21, *"Basi matendo ya mwili ni dhahiri ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na* ***mambo yanayofanana na hayo;*** *katika hayo nawambia mapema, kama nilivyokwisha kuwambia yakwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawata urithi ufalme wa Mungu."*

Tunapokuwa katika tatizo Fulani tunapaswa kuuliza kama **inafanana** na dhambi zilizo onyeshwa.

Kwa mfano, vipi kuhusu uvutaji wa bangi? Je siyo ulevi"? Unaweza pia ukailinganisha na vitu vizuri ambazo zimeonyeshwa.

Angalia orodha hii katika Wagal. 5:22-23, *"Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria."*

Je swala lipo katika swali zaidi ya "tunda la Roho" (hiyo ambayo ni nzuri) au "matendo ya mwili" (yale ambayo ni mabaya)?

Swali lingine la kuangalia...

Je Inaumiza Dhamiri Yako?

Umuhimu wa dhamiri njema.

Kwa ajili ya maandiko yafuatayo:

- 1 Tim. 1:5, "*Walakini mwisho wa agizo hilo ni upendo utokao katika moyo safi na dhamiri njema, na imani isiyo na unafiki."*
- 1 Tim. 1:18-19, "*Mwanangu Timotheo nakukabidhi agizo hilo liwe akiba, kwa ajili ya maneno ya unabii yaliyotangulia juu yako ili katika hayo uvipige vile vita vizuri; uwe mwenye imani na dhamira njema ambayo wengine wameisukumia mbali, wakaangamia kwa habari ya imani."*

- 1 Tim. 3:9, *"Wakiishika siri ya imani katika dhamiri safi."*
- 1 Tim. 4:1-2, *"Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani wakisikiliza Roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani; kwa unafiki wa watu wasemao uongo, wakichomwa moto dhamiri zao wenyewe."*

Hii itatusaidia kwa uzuri kushukuru Warumi 14: 23, "*Lakini aliye na shaka, kama akila, amehukumiwa kuwa na hatia, kwa maana hakula kwa imani. Na kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi."*

Unapofanya kitu ukiwa na mashaka haki yake ni kuharibu dhamiri yako.

Hiyo, anachosema Paulo ni dhambi!

Sasa tendo lenyewe linaweza likawa zuri kipekee, lakini, ukifikiria kuwa ni kosa (kwa sababu ya uelewa mzuri), au ukiwa na shaka juu ya uhalali wake, usifanye!

Usaidizi mwingine...

Wakristo Waliyo Komaa Wanasemaje Kuhusu Swala Hili?

Hii, hasa, haiwezi ikawa mwisho wa kupambanua, kwa sababu Mkristo aliye komaa anawe kukosea; kama wanaweza kuwa wa kwanza kutamka.

Lakini Waeb. 5:14 inasema kwamba hao kwa "kutumiwa" wako katika nafasi ya kupambanua."

Waeb. 5:14, *"Lakini chakula kigumu ni cha watu wazima, ambao akili zao kwa kutumiwa, zimezoezwa kupambanua mema na mabaya."*

Hii ndiyo maana ushauri wa Wakristo waliokomaa huwa inasaidia.

Wafil. 3:17, *"Ndugu zangu mnifuate mimi mkawatazame wao waendao kwa kuufuata mfano tuliowapa ninyi."*

Mfano wa Rehoboamu kushindwa kusikia ushauri wa wakubwa, watu waliokomaa wanaweza kutufundisha kitu.

1 Wafalme 12:6-21, *"Mfalme Rehoboamu akataka shauri la wazee waliokuwa waki simama mbele ya Sulemani, baba yake alipokuwa hai, akasema mwanipa shauri gani ili niwajibu watu hawa? Wakamwambia wakasema, ukikubali kuwa mtumishi wa watu hawa leo, na kuwatumikia, na kuwajibu, na kuwapa maneno mazuri, basi watakuwa watumishi wako daima. Lakini akaliacha shauri lile la wazee, walilompa, akataka shauri kwa wale vijana waliokua pamoja naye na kusimama mbele yake. Akawaambia mwanipa shauri gani ili niwajibu watu hawa, waliosema*

name wakinena utufanyie jepesi kongwa lile alilotutwika baba yako? Na wale vijana waliokuwa pamoja naye wakamwambia wakasema, uwambie hivi watu wale waliokuambia, wakisema, baba yako alilifanya zito kongwa letu, bali wewe utufanyie jepesi, uwaambie hivi, kidole changu cha mwisho ni kinene kuliko kiuno cha baba yangu. Basi kama vile baba yangu alivyowatwika kongwa zito, mimi nitaongeza kongwa lenu; baba yangu aliwapiga kwa mijeledi, bali mimi nitawapigeni kwa nge. Basi, Yeroboamu na watu wote wakamfikia Rehoboamu siku ya tatu, kama mfalme alivyoamuru akisema, mnirudie siku ya tatu. Mfalme akawajibu watu wale kwa ukali, akaliacha shauri lile wazee walilompa; akawajibu kama vile walivyomshauri, vijana, akasema, baba yangu alilifanya zito kongwa lenu, bali mimi nitaongeza kongwa lenu, baba yangu aliwapiga kwa mijeledi bali mimi nitawapiga kwa nge. Basi mfalme hakuwasikia wale watu; maana jambo hili lilitoka kwa BWANA, ili alitimize neno lake, BWANA alilomwambia Yeroboamu mwana wa Nebati, kwa kinywa cha Ahiya Mshiloni. Basi Israeli wote walipoona ya kuwa mfalme hakuwasikia, hao watu walimjibu mfalme, wakasema, tunasehemu gani katika Daudi? Wala ,itunze nyumba yako mwenyewe, Ee Daudi. Hivyo, Israeli wakaenda zao hemani kwao. Lakini kwa habari za wana wa Israeli waliokaa katika miji ya Yuda, Rehoboamu aliwatawala wao. Ndipo mfalme Rehoboamu akampeleka Adoramu, aliyekuwa juu ya shokoa, nao Israeli wote wakampiga kwa mawe hata akafa. Mfalme Rehoboamu akafanya haraka kupanda katika gari, ili akimbilie Yerusalemu. Vivyo Israeli wakaasi juu ya nyumba ya Daudi hata leo. Ikawa, Israeli wote waliposikia ya kwamba Yeroboamu amerudi wakapeleka watu wakamwita aje mkutanoni, wakamfanya mfalme juu ya Israeli mwote, wala hapakuwa na mtu aliyeshikamana na nyumba ya Daudi, ila kabila la Yuda peke yake. Hata Yeroboamu alipofika Yerusalemu, akakusanya nyumba yote ya Yuda, pamoja na kabila la Benyamini, watu wateule mia na themanini elfu, waliokuwa watu wa vita, ili wapigane na nyumba ya Israeli, waurudishe ufalme tena kwa Rehoboamu, mwana wa Sulemani."

Paulo alimfundisha Tito kuwa wadogo wajifunze kwa wakubwa.

Tito 2:3-5, *"Vivyo hivyo na wazee wa kike wawe na mwenendo wa utakatifu; wasiwe wasingiziaji, wasiwe wenye kutumia mvinyo nyingi, bali wafundishao mema; ili wawatie wanawake vijana akili, wawapende waume zao, na kuwapenda watoto wao; na kuwa wenye kiasi, kuwa safi, kufanya kazi nyumbani mwao, kuwa wema, kuwatii waume zao wenyewe, ili neno la Mungu lisitukanwe."*

Alafu swali ambalo kila mara halizingatiwi…

Je Inazuia Uwezo Wako?

Mifano yote na maneno. Paulo anahimiza umuhimu wakuhusina na uwezo wetu kwa wengine.

Angalia kuhusiana kwake na jinsi uwezo wake ulivyo wasaidia wengine.

1 Wakor. 9:19-23, *"Maana ingawa nimekuwa huru kwa watu wote, nalijifanya mtumwa wa wote, ili nipate watu wengi zaidi. Nalikuwa kama Myahudi wa Wayahudi, ili niwapate Wayahudi; kwa wale waliochini ya sheria nalikuwa kama chini ya sheria (ingawa mimi mwenyewe si chini ya sheria), ili niwapate waliochini ya sheria. Kwa walewasio na sheria nalikuwa kama sina sheria, (si kwamba sina sheria mbele za Mungu, bali mwenye sheria mbele za Kristo), ili niwapate hao wasio na sheria. Kwa wanyonge nalikuwa mnyonge, ili niwapate wanyonge. Nimekuwa hali zote kwa watu wote, ili kwa njia zote nipate kuwaokoa watu. Nami nafanya mambo yote kwa ajili ya injili ili kuishiriki pamoja na wengine."*

Alafu anaamuru tufanye vivyo ivyo, katika hilo tunafuata mfano wa Kristo.

1 Wakor. 10:31-11:1, *"Basi mlapo au mnywapo, au mtendapo neno lolote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu. Msiwakoseshe Wayahudi wala Wayunani wala kanisa la Mungu, vile vile kama mimi niwapendavyo watu wote katika mambo yote, nisitake faida yangu mwenyewe, ila faida yao walio wengi, wapate kuokolewa. Mnifuate mimi kama mimi ninavyomfuata Kristo."*

Petro alifundisha uthamani wa kuwa mfano bora kwa kumsaidia mwanamke amlete mume wake kwa Bwana.

1 Petr. 3:1-2, *"Kadhalika ninyi wake, watiini waume zenu kusudi ikiwa wako wasioliamini Neno, wavutwe kwa mwenendo wa wake zao, pasipo lile neno; wakiutazama mwenendo wenu safi na wa hofu."*

Kinachosemwa ni kwamba mfano wa mwanamke inatakiwa iwe kweli sawa na mfano wa mkristo.

Sasa tunatakiwa tuhusike kama swali hili linatusaidia au linabana mvuto wetu kwa Bwana.

Je ni Utumishi Mbaya?

Kwamba sisi ni "watumishi" wa wakati wetu, pesa, na miili ni dhahiri kutoka kwa:

Mfano wa Bwana wa Talanta.

Math.25:14-30, "Maana ni mfano wa mtu atakaye kusafiri, aliwaita watumwa wake akaweka kwao mali zake. Akampa mmoja talanta tano,

na mmoja talanta mbili, na mmoja talanta moja, kila mtu kwa kadiri ya uwezo wake akasafiri. Mara Yule aliyepokea talanta tano akaenda akafanya biashara nazo, akachuma faida talanta nyingine tano. Vile vile na Yule mwenye mbili, yeye naye akachuma nyingine mbili faida. Lakini Yule aliyepokea moja alikwenda akafukua chini, akaificha fedha ya bwana wake. Baada ya siku nyingi akaja bwana wa watumwa wale, akafanya hesabu nao. Akaja Yule aliyepokea talanta tano, akaleta nyingine talanta nyingine tano, akisema Bwana uliweka kwangu talanta tano tazama talanta nyingine tano nilizopata faida. Bwana wake akamwambia, vema, mtumwa mwema na mwaminifu ulikuwa mwaminifu kwa machache nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako. Akaja na Yule aliyepokea talanta mbili, akasema, Bwana uliweka kwangu talanta mbili, tazama talanta nyingine mbili nilizopata faida. Bwana wake akamwambia, vema mtumwa mwema na mwaminifu, ulikuwa mwaminifu kwa machache nitakuweka juu ya mengi, ingia katika furaha ya bwana wako. Akaja na Yule aliyepokea talanta moja, akasema bwana nalitambua ya kuwa wewe u mtu mgumu, wavuna usipopanda, wakusanya usipotawanya, basi nikaogopa nikaenda nikaificha talanta yako katika ardhi; tazama unayo iliyo yako. Bwana wake akajibu akamwambia, wewe mtumwa mbaya na mlegevu ulijua ya kuwa navuna nisipopanda, nakusanya nisipotawanya, basi ilikupasa kuiweka fedha yangu kwa watoa riba, name nikija ningelipata iliyo yangu na faida yake. Basi mnyang'anyeni talanta hiyo, mpeni Yule aliye nazo talanta kumi. Kwa maana kila mwenye kitu atapewa, na kuongezewa tele, lakini asiye na kitu hata kile alicho nacho atanyang'anywa. Na mtumwa Yule asiyefaa mtupeni mbali katika giza la nje; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno."

Maelekezo ya Paulo kuhusu miili yetu.

1 Wakor. 6:19-20, "*Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu mliyopewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi mtukuzeni Mungu katika miili yenu."*

Maelekezo yake kwa wale matajiri wa ulimwengu huu.

1 Tim. 6:17-19, *"Walio matajiri wa ulimwengu wa sasa uwaagize wasijivune, wala wasiutumainie utajiri usio yakini bali wamtumaini Mungu atupaye vitu vyote kwa wingi ili tuvitumie kwa furaha. Watende mema, wawe matajiri kwa kutenda mema, wawe tayari kwa kutoa mali zao, washirikiane na wengine kwa moyo. Huku wakijiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ili wapate uzima ulio kweli kweli."*

Lazima tuweke akilini kwamba muda ni mfupi kwa hiyo nafasi lazima iandaliwe na kutunzwa.

- Waef. 5:16, *"Mkiukomboa wakati, kwa sababu siku hizi ni za uovu."*
- Math. 6:33, *"Tafuteni kwanza ufalme wa Mungu na haki yake; na hivi vyote mtazidishiwa."*

Mwisho tunaweza kuuliza...

Je Yesu anaweza kulifanya?

Kumbuka lengo la utumwa...

Inapatikana katika Luka 6:40, "*Mwanafunzi hawi mkuu kuliko mwalimu wake lakini kila mtu ambaye amehitimu hulingana na mwalimu wake."* Kuwa kama Yesu!

"Yesu anaweza kulifanya?" kuna swali la msingi.

Kama unafikiria hawezi kufanya, basi ni makosa!

Hii inafanya somo la Yesu kuwa la msingi na muhimu katika maisha yetu. Kujifunza maisha yake, mifano yake, neno lake, ilikwamba tuwe na "Nia ya Kristo."

Wafil. 2:5, *"Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ili kuwemo pia ndani ya Kristo Yesu."*

Hitimisho

Ni matumaini yangu kuwa maswali haya saba yanaweza kusaidia ili utambue yaliyo mema na mabaya.

Umuhimu wa kutambua kwa uzuri mema na mabaya tunaiona katika mistari ifuatayo 2 Wakor. 6: 16- 7:1, *"Au hamjui ya kuwa yeye aliyeungwa na kahaba ni mwili mmoja naye? Maana asema wale wawili watakuwa mwili mmoja. Lakini yeye aliyeungwa na Bwana ni roho moja naye. Ikimbieni zinaa kila dhambi aitendayo mwanadamu ni nje ya mwili wake, ila yeye afanyaye zinaa hutenda dhambi juu ya mwili wake mwenyewe. Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa dhamani. Sasa basi mtukuzeni Mungu katika miili yenu. Basi kwa habari ya mambo yale mliyoandika ni heri mwanamume asimguse mwanamke."*

Baadhi ya maswali ya kusisimua fikra zako:

- Je kuna mkristo aliyekomaa mabaye unafiri unaweza kwenda kwake kuomba ushauri?

- Unafiki au anahisi kwamba unatoa wazo la kutosha ya matendo yako kwa ajili yaw engine?
- Unajaribu kuwa na dhamira njema kwa yote unayofanya?
- Je utauliza ukiwa katika tatizo “Yesu atafanya nini?”